



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA




HALMASHAURI YA WILAYA YA CHALINZE

(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb: Na. HWC/L.20/03/VOL/VIII/61/ARR

KAMISHNA WA ARDHI MSAIDIZI,
MKOA WA PWANI,
1 MTAA WA ARDHI,
S. L. P 9230,
11477, DAE ES SALAAM.



21.03.2024

**YAH: HISTORIA YA KIWANJA NAMBA 6 NA 7 KITALU "A" LUGOBA
MINDUTULIENI HALMASHAURI YA WILAYA YA CHALINZE**

Tafadhali husika na somo tajwa hapo juu pamoja na barua yako yenye Kumb. Na.Temp LD/305491/6 ya tarehe 25.02.2024 ukisoma pamoja na barua zetu zenye kumb.Na.CHAL/LD/1321/14/JZS ya tarehe 21/08/2018 na ile yenye Kumb.Na. CHAL/LD/1321/16/JZS ya tarehe 11.02.2019.

Kwa mujibu wa kumbukumbu za ofisi, zinaonesha kuwa kiwanja namba 6 na kiwanja namba 7 kitalu "A" Mindutulieni Chalinze, havijawahi kumilikishwa kwa mtu, kampuni au taasisi yoyote wala kuingizwa kwenye mfumo wa kodi (Molis V.3.1).

Aidha nakujulisha kuwa kwa ukaguzi uliofanywa na ofisi tarehe 18.03.2024 inaonesha kuwa eneo la viwanja tajwa limeendelezwa kwa kuzungushiwa wire wa fence, jengo la ofisi ya XYZ, banda la mlinzi, vyoo na makontainer ya kuhifadha "explosives" kwa ajili ya kulipulia miamba.

Aidha nakujulisha pia awali viwanja tajwa hapo juu yililikuwa vimepimwa na kusajiliwa kama kiwanja namba 4 na kiwanja namba 5 vyote kitalu "A" Lugoba Mindutulieni rejea ramani ya upimaji yenye namba E⁷ 75/25 iliyosajiliwa kwa namba 88500 ambayo hivi sasa imefanyiwa marekebisha baada ya kugundua kuwa viwanja tajwa vilikuwa vimeingizwa kwenye mfumo wa kodi na kumilikishwa kwa LUGOBA PETROLEUM FILLING STATION (T) LTD na hii ikapelekea viwanja hivyo kupewa namba mpya na kuwa kiwanja namba 6 na 7 vyote Kitalu "A" Lugoba Mindutulieni huku ikiwa na namba zilizile za awali za usajili.

Kwa mujibu wa kumbukumbu za ofisi eneo hilo linamilikiwa na kampuni ya XYZ Transport LIMITED ambayo ilinunua eneo hilo kutoka kwa wakazi wazawa wa kijiji cha Mindutulieni.

Mwisho nakujulisha kuwa wakati wa ukaguzi, ofisi haikuweza kubaini aina yoyote ya mgogoro katika eneo hilo.

S.L.P 65, CHALINZE 114 Barabara ya Morogoro, 61315 Chalinze Pwani .


Simu: +023 32935403,

Nukushi: 023 32935402, Barua pepe:

dedchalinze@pwani.go.tz

Tovuti: www.chalinzedc.go.tz

Naomba kuwasilisha taarifa hii kwa hatua zaidi.



Ramadhani Possi
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
CHALINZE



Nakala: XYZ TRANSPORT LIMITED,
S.L.P 4241,
DAR ES SALAAM (kwa taarifa na ufuatiliaji)

S.L.P 65, CHALINZE 114 Barabara ya Morogoro, 61315 Chalinze Pwani .
Simu: +023 32935403, Nukuhi: 023 32935402, Barua pepe:
dedchalinze@pwani.go.tz Tovuti: www.chalinedc.go.tz